

Matumizi ya wanafunzi ya simu za mkononi shuleni

Maelezo kwa wazazi na walezi

Marufuku ya simu za mkononi katika shule ya juu yaliyopo sasa

Marufuku ya kutumia simu ya mkononi katika shule za sekondari yanajenga juu kwa marufuku ambayo yapo tayari katika shule za msingi za serikali za NSW.

Marufuku yanatumika wakati wa masomo, wa mapumziko na wa chakula cha mchana. Wanafunzi wanaruhusiwa kubeba simu wakati wanapasafiri kwenda na kutoka shuleni.

Mwalimu mkuu na walimu wanaweza pia kuidhinisha matumizi ya simu za mkononi kwa madhumuni ya elimu au kama sehemu ya marekebisho ya maana kwa kujifunza kwa wanafunzi na ustawi njema zao.

Ili kuunga mkono na utangulizi wa marufuku, Idara ya Elimu ya NSW imeomba shule zote kushauriana na jumuiya zao za mtaa kuhusu chaguzi mbalimbali za kutekeleza.

Chaguzi hizi zilijumuishwa:

Zima na weka mbali: Simu huzimwa na kuwekwa mbali (kawaida katika begi ya mwanafunzi ya shule). Simu hazitumiwi kwa muda mzima wa siku ya shule.

Simu zipo ndani ya kabati za kufungwa: Wanafunzi hawabebi simu nao; zinakaa ndani ya kabati za kufungwa kwa muda mzima wa siku ya shule.

Begi ya simu iliyofungwa: Wanafunzi huweka simu zao ndani ya begi iliyofunguliwa kwa sumaku na hawawezi kutumia simu zao kwa muda mzima wa siku ya shule. Begi zile zinafungwa kwa sumaku mwishoni kwa siku ya shule.

Simu zinakusanywa kwenye ofisi ya mbele: Wanafunzi huweka simu zao katika ofisi ya shule ya mbele mwanzoni wa siku ya shule na hukusanya mwisho wa siku ya shule (au wakati anapoondoka maeneo ya shule).

Simu zinakusanywa mwanzoni mwa somo: Simu zinakusanywa na kuhifadhiwa na mwalimu mwanzoni wa somo, na kupewa tena kwa mwanafunzi mara tu somo likakwisha na/au wakati mwanafunzi anapotoka darasani.

Jumuiya za shule binafsi ziliamua chaguzi gani zingekubali kwa kutekeleza sera ile.

Mawasiliano ya wanafunzi na wazazi na walezi wakati wa saa za shule

Huenda kuna nyakati ambapo wazazi au walezi wanahitaji kuwasiliana na wanafunzi au kinyume chake wakati wa siku ya shule. Wazazi na walezi wanaweza kuwasiliana na shule kupitia ofisi ya shule na wanafunzi wataweza pia kuwasiliana na wazazi au walezi kupitia ofisi ya shule kama ni dharura au haraka.

Huduma ya wakalimani wa simu

Ikiwa unataka maelezo tafadhali piga simu shuleni. Ikiwa unamhitaji mkalimani kukusaidia na swali lako, tafadhali piga simu Huduma ya Wakalimani wa Simu kwa 131 450 na umwombe kwa mkalimani katika lugha yako.

Umwambie mpigaji simu (mwendeshaji) ile nambari ya simu unayotaka kupiga simu na mpigaji simu atapata mkalimai kwenye simu ili kukusaidia na mazungumzo. Hutatozwa kwa huduma hii.

